

# Kutoka Uzinifu Hadi kufikia Utakatifu



**Maisha ya Watakatifu Maria, Taisi,  
Martha na Theodora wa Misri  
Editor: Padri Etienne Sion, M.afr.**

Kipigo chapa cha Mtandao  
2020

**Agape Publications**  
P.O.Box 76021 Dar-es-Salaam  
Simu : + 255 767 342068  
e-mail : [kungwecentre@gmail.com](mailto:kungwecentre@gmail.com)  
[kungwecentre@outlook.com](mailto:kungwecentre@outlook.com)

## Utangulizi

### Usitende dhambi tena

*“Waandishi na Mafarisayo wakamletea mwanamke aliyefumaniwa katika uzinzi, wakamweka katikati. Wakamwambia, ‘Mwalimu, mwanamke huyu amefumaniwa alipokuwa akizini. Basi katika torati, Musa alituumuru kuwapiga kwa mawe wanawake namna hii; nawe wasemaje?’ Nao wakasema neno hilo wakimjaribu, ili wapate sababu ya kumshitaki. Lakini Yesu akainama, akaandika kwa kidole chake katika nchi. Wao walipozidi kumhoji, alijiinua, akawaambia, ‘Yeye asiye na dhambi miongoni mwenu na awe wa kwanza kumtupia jiwe.’ Akainama tena, akaandika kwa kidole chake katika nchi. Nao waliposikia, wakashitakiwa na dhamiri zao, wakatoka mmoja mmoja, wakianza tangu wazee hata wa mwisho wao; akabaki Yesu peke yake, na yule mwanamke amesimama katikati. Yesu akajiinua asimwone mtu ila yule mwanamke, akamwambia, ‘Mwanamke, wako wapi wale washitaki wako? Hakuna aliyekuhukumu kuwa na hatia?’ Akamwambia, ‘Hakuna, Bwana.’ Yesu akamwambia, ‘Wala mimi sikuhukumu. Enenda zako, wala usitende dhambi tena.’» Yoh 8:3-11.*

### Usitende dhambi tena.

Hatujui kama mwanamke huyu amerudia dhambi ya uzinifu au sivyo. Yohane hakuandika habari zake baadaye. Lakini tunajua kwamba Maria Magdalena baada ya kukutana na Yesu, alibadilisha maisha yake yote. Aliacha uasherati wake ili kumfuata na kumtumikia Yesu. Luka anatusimulia kwamba siku moja Yesu alipoalikwa kula karamu na Farisayo mmoja, kwa jina Simoni, Mwanamke mzinifu<sup>1</sup> aliingia chumbani na *“akasimama nyuma karibu na miguu yake, akilia, akaanza kumdondoshea miguu machozi yake, na kuipangusa kwa nyuwele za kichwa chake, akiibusubusu miguu yake na kuipaka yale marhamu.”* Lk 7:38. Alionyesha toba kweli, bila kuona haya mbele ya watu, na akampatia Yesu maisha yake yote. Machozi yanamaanisha moyo wake, nywele zinamaanisha mwili wake, marhamu inamaanisha kazi na mali yake yote.

---

<sup>1</sup> Mwanamke huyu anaweza kuwa Maria Magdalena.

Watakatifu wengi walimfuata mfano wa Maria Magdalena, wa zamani na wa siku hizi, kama Mt Augustino wa Hippone, Mt Pelagia au Mt. Charles de Foucauld,

Wanawake hawa, Maria, Taisi, Martha na Theodora, ambao tunaandika maisha yao, walitenda dhambi za uasherati na uzinifu, kila mmoja kwa namna yake. Walipoguswa na neema ya Mungu na kukutana na Yesu kwa njia ya ki-roho, hawakuacha dhambi zao tu, kadiri ya maneno ya Yesu, "*usitende dhambi tena*", bali walianza kuishi tofauti na kufanya toba maishani mwao mwote. Mungu akawabadilisha na wakawa watakatifu.

Simulizi za maisha yao zimeandikwa zamani na watu tofauti tofauti. Habari za Maria wa Misri zimeandikwa na Sophronius Askofu wa Yerusalemu, kabla ya mwaka 636. Habari za Taisi zimeandikwa katika karne la IV na mtu asiyejulikana. Habari za Theodora zinapatikana katika '*The Golden Legend*' iliyoandikwa na Yakobo de Voragine. Zimulizi hizo zilitafsiriwa kwa lugha mbalimbali. Wakristo wengi ulimwenguni walivutwa na maisha yao.

Natumaini kwamba Wakristo wengi wanaojua tu lugha la Kiswahili watafurahi kuzisoma habari zao na kukuguswa moyoni mwao, hata kuziacha dhambi za uasherati na uzinzi na kuanza kuishi katika usafi wa moyo kwa ajili ya Yesu. Pia wavutwe na mifano ya wanawake hawa kufanya toba kwa ajili ya dhambi zao na kwa ajili ya dhambi za ulimwengu.

Padri Heribert Meyer ametafsiri simulizi za maisha ya Watakatifu Maria na Taisi, mnamo mwaka 1947. Nimebaki na tafsiri hiyo, isipokuwa nimebadilisha machache ili Kiswahili kilingane na Kiswahili cha kisasa. Pia nimejitahidi kutafsiri maisha ya Mt. Theodora kutokana na simulizi tunayopata katika '*the Golden Legend*', maisha ya Mt. Martha kutokana na *Ethiopian Synaxarium*, Kitabu cha Watakatifu wa Kanisa la Orthodoksi, Ethiopia, na Mt. Pa'esa kutokana na *Coptic Synaxarium*, Misri. Mungu awabariki sana.

Fr. Etienne Sion M.afr.

# Mtakatifu Maria wa Misri



**Mtubu**

Alikuwako padre mtawa katika monasteri fulani nchi ya Palestina waliyokaa zamani Wayahudi. Padre huyu alikuwa mwenye fadhila bora sana. Jina lake lilikuwa Zosima. Aliletwa utawani alipokuwa bado mtoto mdogo akafundishwa vizuri kazi zote za utawa. Akashika kwa uaminifu sheria zote na taratibu za utawa. Akawapita wenzake wote katika juhudi ya kujikana. Juu ya magumu waliyoamriwa watawa wote aliongeza mengine, ili atishe mwili wake na tamaa zake. Watawa wenzake wote hawakumwona amekosa yoyote. Akawa mfano wa fadhila zote kwa watawa wenzake. Mara nyingi watawa wageni, waliotoka nchi za mbali, walikuja katika monasteri ile wakitaka kuona mfano wake na kuyasikia mafundisho yake.

Zosima alikuwa anawaza maneno ya Mungu kila wakati. Usiku akipumzika katika mkeka wake na mchana akifanya kazi hata akila chakula hakuacha kusali zaburi. Mara nyingi alifumbuliwa mambo ya siri akaona matokeo ya Mungu. Mwana wa Mungu mwenyewe amesema kwamba heri yao wenye moyo safi, kwani watamwona Mungu. Naye Zosima huyu akajitahidi kuwa na moyo safi, akatakasa roho yake kwa kufunga na kukesha. Kwa hivi akastahili kuyaonja kidogo hapa duniani aliyowekewa tayari mbinguni kwa hisani ya Mungu.

Zosima alikaa katika monasteri ile mpaka alipotimia umri wa miaka hamsini na mitatu. Hapo yalimtokea mawazo ya majivuno. Akawa anafikiri kwamba ni mtu mkamilifu sana asiyehitaji kufundishwa na wenzake. Zosima mwenyewe alisimulia baadaye kwamba aliwaza hivi: "Hayuko mtawa mwingine duniani hapa anayeweza kunifundisha mambo ya ukamilifu nisiyojua mimi. Hayuko mtawa anayeweza kuniagiza kazi ya roho nisiyotimiza bado." Basi siku moja alipokuwa anawaza hivi alisikia anaambiwa maneno haya moyoni mwake: "Zosima, umepigana vizuri kwa kadiri ya nguvu zako. Umetimiza vizuri lazima zako za utawa. Lakini kila mtu asijione mwenyewe kuwa mkamilifu. Mapigano utakayopata mbele bila kuyajua ni magumu zaidi kuliko yale uliyokwisha shinda. Ninataka kukuonyesha njia nyingine za wokovu zilizo bora zaidi kuliko njia yako. Basi ufanye kama baba Abraham, utoke katika nchi yako na uache jamaa yako ukatoke katika nyumba ya baba yako (Mwa 12:1). Nenda ukakae katika monasteri uliyo kando ya Yordani!"

Zosima hakukawia kutimiza amri hiyo. Akatoka katika monasteri yake akaenda kwenye mto Yordani. Akaongozwa na Yule aliyesema naye akafika kwenye monasteri ile. Akagonga mlango akaongea kwanza na mngoja mlango. Huyu akampasha habari abate wa monasteri. Abate akampokea Zosima kwa wema akatambua upesi kuwa Zosima ni mtawa. Basi wote wawili wakapiga magoti wakasali kama ilivyokuwa desturi. Baadaye abate akamuliza Zosima akasema: "Umetoka wapi ndugu?" Zosima akajibu: "Ninafikiri kuwa

si lazima kutaja mahali nilipotoka. Lakini nimewafikia ninyi ili nijifunze kwenu, baba! Nimesikia mnasifiwa juu ya maajabu yenu, kwamba mnaunganisha roho zenu na Mungu." Abate akajibu: "Mungu mwenye kuponya magonjwa akufundishe wewe, ndugu, na sisi pia kushika amri zake. Atusaidie kutenda yanayompendeza. Wanadamu hawawezi kuwafundisha wenzao wasipojiangalia wenyewe. Yawapasa kutumia neema wanazopewa na Mungu na kufanya kazi pamoja naye, ili waokoke. Kwa kuwa Kristo amekuongoza na amekuleta katika monasteri yetu upate kujifunza, basi ukae hapa, usituache! Mchungaji mwema aliyetoa uzima wake kwa ajili yetu anamwita kila kondoo kwa jina lake. Yeye atulishe sisi sote kwa neema za Roho Mtakatifu." Zosima akapiga magoti na abate akasali juu yake akampokea katika monasteri yake.

Zosima akaona watawa wazee wenye fadhila bora wanaomtumikia Mungu kwa mioyo yao yote. Katika kanisa lao walimsifu Mungu mchana na usiku. Yalikuwa makundi mbalimbali ya watawa yaliyopokezana kwa kadiri ya taratibu yao. Mchana walifanya kazi kwa mikono kila wakati na kwa midomo yao walisali zaburi bila kuchoka. Zosima hakuwasikia watawa wanaoongea maneno ya bure (Mt 12:36). Hata kwa mawazo yao hawakufikiri mambo ya dunia (Kol 3:2), bali kila mmoja alijitahidi kuiacha dunia na mambo yake na furaha zake. Chakula cha roho zao kilikuwa neno la Mungu (Mt 4:4/Kum 8:3). Wakatuliza njaa ya miili yao kwa mikate na kwa maji. Wakawa na matumaini kupata huruma ya Mungu kwa ajili ya masumbuko haya waliyovumilia.

Zosima alipoona bidii ya watawa hawa alifurahi sana. Akajitahidi kufuata mifano yao na kujipatia ukamilifu. Watawa wote walisaidiwa katika juhudi yao kwa upweke wa nyumba yao. Nyumba hii ilikuwa mbali sana ya miji katika jangwa kando ya Yordani. Kwa sababu hii hawakufikiwa na wageni. Mlango wa monasteri ulikuwa umefungwa kila wakati. Hivyo watawa hawakuudhiwa kwa maneno ya wageni wadadisi.

Katika monasteri hiyo desturi ya pekee ilishikwa tangu zamani. Kila mara Dominika ya kwanza ya Kwaresima watawa wote walihudhuria misa takatifu na kila mmoja alipokea komunio takatifu, ndiyo mwili wa Bwana Wetu Yesu Kristo. Kwisha misa walikula chakula kidogo. Baadaye walikusanyika tena katika kanisa lao wakasali pamoja. Halafu kila mtawa alimwaga abate akimkumbatia na kumsujudia kwa kuomba baraka yake. Walipokwisha agana wao kwa wao mlango wa utawa ulifunguliwa na watawa wote walitoka pamoja kwa maandamano wakiimba: "*Bwana ni nuru yangu na wokovu wangu, nimwogope nani? Bwana ni ngome ya uzima wangu, nimhofu nani?*" Zab 27:1. Basi watawa wote wakatoka utawani isipokuwa walinzi wawili watatu. Walinzi hawa walibaki utawani si kwa kulinda mali zao, maana

hawakuwa na mali yo yote, ila kazi yao ilikuwa kusali kanisani mpaka watakaporudi wenzao. Kila mtawa alichukua masurufu kwa kadiri alivyopenda mwenyewe, yaani mikate au tini au tende au mboga. Wengine hawakuchukua chakula cho chote, maana hawa waliridhika na majani na mizizi waliyoona jangwani. Kila mtawa alichukua masurufu yake kwa siri isije mwenzake akajua jinsi alivyofunga wakati wa Kwaresima.

Walipokwisha toka monasterini wote walivuka Yordani na walipofika ng'ambo yake waliachana. Kila mmoja alikwenda peke yake mahali alipotaka mwenyewe. Akimwona mwenzake kwa mbali anamwepuka na anakwenda pengine. Kila mtawa alikaa peke yake usoni pa Mungu. Lakini hata jangwani walishika taratibu ya nyumbani kwao, wakaimba zaburi saa zile zile zilizoamriwa, wakala chakula wakati wake. Walikaa hivi jangwani siku zote za Kwaresima mpaka Jumatano inayotangulia siku ya Alhamisi Kuu. Jumatano ile walikutana tena katika monasteri. Mungu peke yake alishuhudia matendo na masumbuko ya kila mtawa, wala hawakusimuliana yo yote iliyowatukia jangwani.

Hii ilikuwa sheria katika monasteri hii nayo ilishikwa na watawa wote. Kila mtawa alijitiisha mwenyewe machoni pa Mungu apate kumpendeza yeye, siyo watu (Mt 6:1). Walijua kuwa yote tunayotenda kuwapendeza wanadamu hayatufaidii kitu, bali yatuhasiri. Kwa kadiri ya sheria hii Zosima pia alitoka monasterini akaenda jangwani ng'ambo ya Yordani. Akachukua masurufu kidogo kadiri ya mahitaji ya mwili wake. Akafanya vile kama wenzake. Aliingia jangwani akasali zaburi saa ile iliyoamriwa na taratibu ya monasteri akala chakula kidogo wakati wake. Usiku aliketi chini katika mchanga akapumzika na kulala usingizi kwa muda mfupi pale pale alipofika lilipotua jua. Asubuhi na mapema aliamka akaendelea jangwani.

Alipoanza safari yake ya jangwani alikuwa anatumaini kwamba atamkuta mkaa pweke. Akawa na nia ya kujifunza kwake na kukuza roho yake. Akasafiri jangwani kama anayemwendea mtu fulani. Akatembea hivi siku ishirini bila kumwona mtu. Siku hiyo saa sita ya mchana alisimama akasali ibada ya saa sita akaelekea upande wa Mashariki. Akaimba zaburi akisimama wima, akaelekeza macho mbinguni. Mara aliona upande wa kuume mfano wa mtu. Akashtuka kwanza maana alifikiri kwamba ameona kizuka cha shetani. Akajiandikia ishara ya msalaba akafukuza hofu yake. Alipomaliza ibada yake alitazama, akaona kweli ni mwanadamu aliyekimbia upande wa Magharibi. Naye mwanadamu huyu alikuwa mwanamke. Ngozi yake ilikuwa nyeusi kwa sababu ya jua. Nywele zake zilikuwa nyeupe kabisa kama pamba zimeteremka mpaka mabegani.

Zosima aliyependa kukutana na mkaa pweke jangwani mle alifurahi sana. Akamfuata mtu yule akapiga mbio. Zosima alikuwa amejaa furaha, maana siku zote tangu alipotoka utawani hakumwona mtu wala kindege wala mnyama. Sasa alitaka kujua ni mtu gani, akawa anatumaini atapata faida kwa roho yake. Lakini mwanamke alipoona kuwa Zosima anamkaribia, alianza kukimbia akapiga mbio. Pia Zosima akazidi kukaza mwendo wake bila kukumbuka uchovu wake. Lakini kwa kadiri alivyozidi kumfuata mbio na mwanamke alizidi kukimbia. Zosima alikuwa na nguvu zaidi kuliko mwanamke akapata kumkaribia polepole. Alipomkaribia kidogo alipaza sauti akamwita hali analia machozi akasema: "Ee mtumishi wa Mungu, kwa sababu gani unakimbia? Mbona mimi ni mzee na mkosefu. Ninakuomba kwa ajili ya Mungu usimame! Ninajua kuwa unakaa jangwani kwa ajili ya Mungu. Uningoje mimi mkosefu nisiyestahili kukuona. Uningoje kwa ajili ya tuzo yako unayotumaini kupewa kwa sababu ya taabu ulizovumilia jangwani humu. Usimame, unisalie na unibariki mimi mzee. Ninakutaja kwa ajili ya Mungu, usimame!"

Wakati walipofukuzana hivyo walifika mahali palipofanana na mto. Zosima alidhani kuwa ni mto mpana kidogo akasimama. Lakini mwanamke akavuka akafika ng'ambo ya pili. Zosima akatokwa na machozi nayo yalianguka chini. Akalia kwa sauti na mlio wake ukasikilika mbali sana.

Mwanamke hali anakimbia alimjibu Zosima akasema: "Baba Zosima, uniwie radhi kwa ajili ya upendo wa Mungu! Siwezi kukuelekea wewe wala kujionyesha kwako. Maana mimi ni mwanamke wala sina nguo ya kujifunika. Basi, ukikubali kwa hisani yako, mimi mkosefu niongee nawe, ninaomba unitupie bushuti yako ili nikuelekee nipate baraka yako!"

Zosima hakuwa mwoga, lakini aliposikia maneno ya mwanamke huyu alishtuka sana. Ijapokuwa mwanamke huyu hajamwona hata mara moja wala hajasikia habari zake, alimwita kwa jina lake. Hakuweza kujua jina hili isipokuwa amelifumbiliwa kwa mwangaza wa Roho Mtakatifu. Basi Zosima akavua bushuti yake akamtupia akitazama upande alitokea. Mwanamke akaiokota akajifunika akamwambia: "Baba, kweli wewe unataka kuniona mimi mkosefu? Unataka kuona na kujifunza nini? Mbona umesumbuka bure kufika jangwani hapa!" Zosima akamsujudia mwanamke akaomba baraka kama ilivyokuwa desturi. Naye mwanamke mzee akamsujudia Zosima akaiomba baraka. Wakawa wamesujudiana na kuombana baraka. Zikapita saa kadha wa kadha nao bado wamesujudiana. Mwisho mwanambe akamwambia Zosima akasema: "Baba Zosima, yakupasa wewe kutoa baraka na kunisalia kwa kuwa wewe ni padre. Tangu miaka mingi unamtumikia Mungu penye altare na umeagizwa kuwagawia watu siri takatifu za Mungu."



Maneno haya ya mwanamke yalizidi kumwogofya na kumhangaisha padre mzee. Akatetemeka na kutoka jasho kwa kuogopa akasema: "Ee Mama, kwa ujuzi huu uliopewa na Mungu unaonyesha wazi kuwa umejifia mwenyewe na umeunganika na Mungu. Umepata wingi wa neema maana umejua jina langu ingawa hujaniona bado hata mara moja. Mungu hupendezwa zaidi na mtu mwenye moyo safi ulipambwa na fadhila kuliko mtu mwenye cheo bora. Kwa sababu hii nakuomba kwa ajili ya pendo la Mungu, unibariki na unisalie kwa sala yako inayompendeza Mungu!"

Mwanamke akamwonea huruma padre mzee asilegea kwa unyenyekevu. Akambariki akasema: "Atukuzwe Bwana, mwenye kuwaongoza watu kwa wokovu wa milele." Zosima akaitikia akasema: "Amina." Basi hapo wote wawili wakasimama. Mwanamke akamwambia Zosima akasema: "Ewe mtumishi wa Mungu, kwa sababu gani umenifikia mimi mwanamke mkosefu? Lakini ninajua kuwa Roho Mtakatifu amekuongoza mpaka hapa upate kunisaidia uhitaji wangu. Lakini unisimulie kwanza habari za Kanisa takatifu hapa duniani. Tena nani anatawala sasa duniani? Nani anachunga kundi la Kanisa?" Zosima akamjibu akasema: "Mama, kwa maombezi yako Mungu amelijalia Kanisa kuwa na amani ya kudumu. Lakini usikatae sasa ombi langu, maana mimi ni mtawa mzembe kabisa. Usali kwa stahili ya Mkombozi wetu kwa ajili ya dunia nzima. Uniombe mimi, ili safari yangu ya kufika jangwani hapa isiwe bila mafanikio kwa roho yangu nyonge!"

Mwanamke akamjibu akasema: "Wewe, baba Zosima, umepata cheo cha upadre. Yakupasa wewe kuwaombea watu wote, pia mimi. Maana hii ni kazi kubwa ya kila padre. Lakini kwa kutimiza amri yako nitafanya yote uliyoniamuru." Akaelekea upande wa matokeo jua, akainua macho mbinguni akapanua mikono akasali kimya. Zosima akaona jinsi anavyotikisa midomo yake, lakini hakusikia neno. Akasimama karibu yake, akatetemeka akakaza macho chini wala hakuthubutu kusema neno. Mwanamke akaendelea kusali kwa muda mrefu. Basi Zosima akainua macho kidogo. Akaona kuwa mwanamke miguu yake haikusimama chini, bali imeinuliwa juu kadiri ya mkono mmoja. Zosima alipoona ajabu hili alihofu zaidi akajitupa chini akatokwa na jasho la kuogopa. Akasali moyoni mwake akasema: "*Ee Bwana, unihurumie!*" Lk 18:13.

Zosima alipokuwa amelala hivi alianza kuwaza vibaya juu ya mwanamke. Alidhani kwamba mwanamke ni pepo mbaya anayejisingizia kusali. Papo hapo mwanamke akamwelekea Zosima, akamwamsha akasema: "Baba, kwa sababu gani mawazo haya yanahangaisha moyo wako? Na kwa sababu gani unawaza mabaya kwamba mimi ni pepo mbaya na ninajisingizia kusali? Basi, baba, ujue kwamba mimi ni mwanamke mkosefu ijapokuwa nimepata ubatizo.

Mimi si pepo, ninao mwili ulio vumbi na majivu. Sina shughuli na pepo wabaya." Akajiandikia alama ya msalaba katika paji la uso na macho na midomo na kifua, akasema: "Ee baba Zosima, Mungu atukinge na adui mbaya na mashauri yake, kwani hutuchukia sana."

Mzee Zosima aliposikia maneno haya alijianguka tena penye miguu yake akasema: "Ninakuomba kwa ajili ya Bwana wetu Yesu Kristo aliyependa kuzaliwa na Bikira, unisikilize. Kwa ajili yake umeingia ukiwa huu na unajisumbua hivi. Usinifiche jina lako na uniambie nyumbani kwako ni wapi? Unihesabie miaka yote uliyokaa upwekeni humu. Lakini ninaomba unisimulie habari zako zote upate kufumbua maajabu makubwa ya Mungu. Maana katika Maandiko Mtakatifu imeandikwa hivi: *'Hekima iliyofumbwa na hazina zisizoonekana vinafaa nini?'* Unisimulie yote, si kwa kujivuna wala kujisifu bali kwa kunifurahisha mimi mkosefu. Ninadhani kwamba Mungu ameniongoza jangwani mpaka kwako hapa, kusudi awafumbulie watu habari zako. Kama asingalitaka kuyafumbua maajabu yake hangalikubali wewe ukutane na mtu, wala hangalinitia moyo wa kuvumilia masumbuko ya safari hii."

Basi mwanamke akamwamsha baba Zosima akasema: "Uniwie radhi, baba yangu. Ninaona haya sana kukusimulia maovu mabaya kabisa ya maisha yangu. Lakini nitakufumbua aibu yangu upate kutambua jinsi roho yangu ilivyokuwa imezama katika uasherati. Kweli, siwezi kusimulia habari zangu kwa kujisifu. Nitawezaje kujivuna? Mbona nalikuwa chombo kiteule cha

Shetani<sup>2</sup>. Nikisimulia maovu yangu yote hutaweza kuyasikiliza. Utanikimbia kama mimi ni nyoka mwenye sumu. Nitakueleza ilivyokuwa. Lakini ninakuomba usichoke kuniomba, ili nistahili kuhurumiwa siku ya hukumu."

Mzee Zosima akalia machozi naye mwanamke akaanza kusimulia habari zake akasema:

"Nimezaliwa nchi ya Misri. Nilipokuwa

msichana mdogo mwenye umri wa miaka kumi na miwili tu nalikataa upendo wa baba na mama<sup>3</sup>. Nikatoroka nyumbani kwao nikaenda Aleksandria. Ole wangu, ewe Baba! Ninaona haya kabisa kukumbuka jinsi nilivyofanya haraka kuharibu ubikira wangu. Nilijitia katika dhambi ya



<sup>2</sup> Paulo alikuwa chombo kiteule mikononi mwa Yesu, Mdo 9:15.

<sup>3</sup> Kama katika Mfano wa mwana mpotevu. Mwana mdogo alimwacha Baba yake na nyumbani mwake ili kuishi maisha ya uasherati, Lk 15:11...

uasherati na tamaa zangu mbaya hazikushiba kamwe. Ninashindwa kukusimulia yote. Nitakusimulia kidogo tu upate kutambua jinsi nilivyowaka moto wa uasherati. Muda wa miaka kumi na saba na zaidi nimeendesha mwendo wa uasherati. Nilitupa ubikira wangu bure, bila kutaka mshahara wa dhambi. Siku zote sikukubali kupokea fedha yo yote ingawa walitaka kunilipa. Tamaa yangu ilikuwa mno kwamba nimekataa fedha, kusudi nifikwiwe na watu wengi zaidi waliotaka kutenda dhambi nami. Lakini usifikiri kuwa sikuhitaji fedha, la! Ilinipasa kuomba 'maskini' na kufanya kazi ya kusokota nyuzi ili nipate riziki zangu. Nalikuwa nalifurahi sana na mwenendo mbaya huu. Niliona bora nilipoweza kugaagaa katika matope machafu ya uasherati.

Basi mwaka fulani wakati wa kiangazi naliona watu wengi sana waliotoka Libia na Misri wanakwenda bandarini. Nikamwuliza kijana nikasema: 'Watu hawa wanakwenda wapi?' Kijana yule akanijibu akasema: 'Wote wanasafiri kwenda Yerusalemu kwa sikukuu ya Utukufu wa Msalaba mtakatifu itakayofanywa baada ya siku chache tu.' Nikauliza mara ya pili nikasema: 'Unafikiri kwamba watanichukua nikitaka kusafiri nao, maana wote ni wanaume tu?' Kijana akasema: 'Ukilipa nauli hawatakukatalia!' Nikajibu: 'Sina nauli wala masurufu. Lakini nataka sana kusafiri nao. Nitaingia katika merikebu yao. Wakitaka kunirudisha basi natajitoa mwenyewe.'

Baba, unisamehe uovu wangu, maana nalitaka kusafiri nao kusudi nipate nafasi nyingi zaidi za kutenda dhambi. Uniwie radhi, baba, nisiendeleo kukusimulia ubaya wangu. Mungu ajua kuwa ninatetemeka nikikumbuka uovu wangu. Hata sasa ninaposimulia habari zangu maneno yangu yamechafua hewa."


Zosima akalia machozi akamwomba akasema: "Endelea kusimulia, mama! Ninakuomba kwa Mungu, timiliza mafundisho yako!" Basi mwanamke akaendelea kusimulia akasema:

"Kijana yule akatambua maana ya maneno yangu, akachekeka akajitokea. Basi nikatupa kazi yangu niliyofanya siku ile nikawafuata vijana wale mpaka bandarini. Nikawakuta vijana wengine kadiri ya kumi, maana wengine walikwisha panda merikebuni. Wote walikuwa vijana wenye nguvu sana na wazuri. Nikawatamani wote kwa kutimiza nia zangu mbaya. Sikuzote nalikuwa sioni haya hata kidogo. Hata siku ile nikawaendea bila haya nikawaambia: 'Mnichukue katika safari yenu, nami sitakuwa na baridi kwenu!' Nikawaambia pia maneno mengine mengi yasiyofaa, nao wakachekeka. Ingawa walikuwa wameona tabia yangu isiyo na adabu walikubali nipande merikebuni. Basi tukafunga safari tukapita baharini. Baba, siwezi kusimulia yaliyotukia baadaye. Ulimi wangu unashindwa kutamka jinsi nilivyowakosesha vijana wengi sana walionikataa kabisa. Nikawa kama

mwalimu wa uasherati kwa wale wasiojua bado dhambi hii. Basi, nisisimulie mengine. Ninashangaa kwa kuwa bahari imevumilia uovu wangu (Yon 1:15) na dunia haikufunguka kunimeza mara moja (Hes 16:31-34), kwa sababu nimepoteza roho za watu wengi sana. Ninafikiri kwamba Mungu alingoja toba yangu, maana hapendi mtu apotee, bali ataka wote waokolewe (Eze 18:3), kwani hafurahii kifo cha mkosefu. Anangoja kwa uvumilivu kuongoka kwetu. Basi, tulifika upesi mjini Yerusalemu. Siku nilizopitisha huko kabla ya sikukuu nalitumia kwa mambo mabaya zaidi kuliko kwanza. Ilikuwa haikunitosha kuwakosesha vijana wale baharini na katika nchi kavu. Hata katika mji mtakatifu niliwatongoza wenyeji na wasafiri wengi sana.

Kulipokucha siku ya sikukuu ya Utukufu wa msalaba mtakatifu nalikusudia kuwashawishi na kuwanasa vijana wengine. Asubuhi na mapema naliwaona wanakwenda kanisani. Nikawafuata kwa haraka nikawakuta mbele ya kanisa. Ilipoanza ibada nilijiingiza katikati ya kundi la watu waliosonga mbele kutaka kuingia kanisani. Pamoja na watu wale nalifika mpaka kwenye lango la kanisa. Nalitaka kuingia kama wenzangu. Lakini sikuweza kuingia. Ilikuwa kama ninarudishwa kwa nguvu. Naliona kama ninasukumwa nyuma. Nikabaki peke yangu mbele ya kanisa. Nikafikiri kwamba labda nimeshindwa kuingia kwa sababu ya udhaifu wangu. Basi nikajiingiza mara ya pili katika kundi jingine la watu waliokaribia. Nakajibidiisha sana kuingia kanisani pamoja na kundi hili la pili. Lakini hata safari hii ya pili nalisumbuka bure, maana nalishindwa vile vile. Nilipofika kwenye lango wote walipita, wakaingia bila shida yo yote. Kwangu mimi ilikuwa kama lango likanikataa. Mara

nikasukumwa sana. Nikawa uwanjani mbele nikajaribu na kila mara Basi nikawa nalijitahidi kwa kanisani bila nyuma kidogo wa uwanja. mwenyewe; kinanizuia mtakatifu. Papo ukashituka sana ya wokovu. nimeshindwa



nyuma kwa nguvu ninasimama tena ya kanisa. Hivyo safari tatu hata nne, nilisukumwa tena. nimechoka, maana nguvu zote kuingia kufaulu. Nikarudi nikajificha mwisho Nikajiuliza kitu gani kuona Msalaba hapo moyo wangu nikapata mawazo Nikatambua kuwa kuingia kanisani

kwa sababu ya dhambi zangu na uasherati wangu. Nikashikwa na uchungu juu ya uovu wangu nikatokwa na machozi. Nikalia ndani ya moyo wangu nikajipiga kifuani kwa majuto juu ya ubaya wangu. Mahali pale niliposimama, kwa juu yake nikaona sanamu ya Mama mtakatifu wa Mungu. Nikaitazama kwa muda mrefu nikasema: 'Ee Bikira mtakatifu, umemzaa Mwana wa Mungu aliyejifanya mtu. Ninajua kuwa mimi mwasherati mchafu sistahili kutazama sanamu yako. Macho yangu yaliyojaa uchafu hayastahili kutazama sanamu yako, maana wewe ni bikira safi mweupe kabisa. Wewe umelinda roho yako na mwili wako bila mawaa siku zote. Wewe uliye Bikira safi kabisa unaweza kunikataa na kunitupa. Lakini nimesikia kuwa Mwana wa Mungu ametwaa ubinadamu apate kuwakomboa wakosefu. Unisaidie, wewe uliyestahili kuwa Mama yake. Nimetupwa, wala sina msaidizi. Usikilize maungamo yangu! Unipatie neema ya kuingia kanisani ili niuone Msalaba mtakatifu ambao Mwanao amekufa juu yake. Wewe Bikira mtakatifu wa daima umemchukua katika mwili wako safi ukamzaa ukawa bikira kama kwanza. Naye amemwaga damu yake apate kunikomboa mimi mwasherati mbaya. Ee Bibi, unipatie neema ya kuingia kanisani ili niabudu Msalaba mtakatifu. Ninakuahidi kwa ajili ya Mwanao Yesu Kristo kuwa sitanajisi tena mwili wangu kwa dhambi ya uasherati hata kidogo. Ndiyo, ee Bikira mtakatifu! Nikijaliwa kuuona na kuuabudu Msalaba wa Mwanao nitaacha dunia na mambo na matendo yake na yote yaliyo ndani yake. Nitaacha dunia na nitakwenda mahali utakaponipeleka wewe, kiongozi na Mama yangu na mdhamini wangu.'

Baada ya kuahidi haya nilijiona nimetulia kidogo nikawa na imani. Nikajaa matumaini na upendo kwa Mama wa Mungu. Nikatoka mahali niliposali nikajiingiza katika kundi jingine la watu walioingia kanisani. Kumbe safari hii sikusukumwa nyuma nilipofika kwenye lango la kanisa. Nikaingia kanisani bila shida. Nikajaliwa kuuona msalaba mtakatifu. Nikatambua jinsi Mungu anavyopenda kuwapokea wakosefu wanaotubu. Nikajitupa chini nikabusu sakafu nikaabudu Msalaba uliotuletea wokovu wetu. Baadaye nikatoka kanisani nikairudia sanamu ya Mama Maria kwa haraka sana. Maana yeye alikuwa sasa kiongozi wangu kwa kutimiza ahadi yangu. Nikapiga magoti mbele ya sanamu yake nikasali nikasema: 'Ee Mama mpole, umenitendea kwa huruma wala hukukataa sala yangu nyonge. Nimeona utukufu wa Mungu ambao sisi wakosefu hatushahili kuuona. Nimeona utukufu wa Mungu Mwenyezi anayepokea mikononi mwako toba na maombi ya wakosefu. Nisemeje, mimi mkosefu mpotevu? Yanipasa sasa kutimiza niliyokuahidi kwa jinsi inavyokupendeza wewe. Ninakuomba uniongoze kwenda mahali unapotaka wewe. Uwe kiongozi wangu nipate kuokoka. Unifundishe ukweli ukaniongoze katika njia ya kutubu!'

Mara nikasikia sauti iliyosema kutoka mbali: 'Nenda ng'ambo ya Yordani. Huko utapata raha!' Nikasadiki kuwa maneno haya yakanipasa mimi. Nikatazama sanamu ya Mama wa Mungu, nikalia machozi nikasema: 'Ee Bibi, ee Mama, ee Malkia wa dunia nzima, wewe unawaletea wanadamu wote wokovu wa milele. Usiniache kamwe!'

Hapo nikatoka katika uwanja wa kanisa kwa haraka. Wakati nilipotoka nalipita karibu ya mtu aliyekwenda kanisani. Huyu aliponiona alinyosha mkono wake akanipa vipande vitatu vya fedha akasema: 'Pokea sadaka hii, bibi!' Nikavipokea nikanunua mikate mitatu, ikawa masurufu ya safari yangu. Nikamwomba mwokaji mikate nikasema: 'Njia ya kwenda Yordani ni wapi?' Akanieleza njia. Nikatoka mjini nikashika njia ya kwenda Yordani. Njiani nikalia machozi wala hayakukauka mpaka nilipofika Yordani kwenyewe.

Ilikuwa saa tatu ya mchana nilipojaliwa kuuona msalaba mtakatifu. Katika safari yangu katika kila mji niliuliza njia ya kuendelea mpaka Yordani. Jua lilianza kutua nilipofika kwenye kanisa la Yohani Mbatizaji mtakatifu lililopo kando ya Yordani. Nikaingia kanisani nakasali. Baadaye nalikwenda mtoni nikaosha mikono na uso wangu. Nikapokea sakramenti ya kitubio na ya Ekaristi takatifu. Baadaye nikala nusu ya mkate niliyochukua nikalala usingizi sakafuni. Kulipokucha nalivuka Yordani. Nikamwomba kiongozi wangu Mama Bikira Maria, aniongoze anipeleke mahali anapopenda mwenyewe. Nikaingia jangwani nikaenda mbali sana kusiko njia, wala watu, wala wanyama. Tangu siku ile mpaka siku ya leo sikutoka tena jangwani. Nikamngojea Yule aokoaye wadogo na wakubwa wenye kumwelekea."

Zosima akamwuliza mwanamke akasema: "Tangu miaka mingapi umekaa jangwani humu?" Mwanamke akajibu: "Nadhani imepita miaka arobaini na saba tangu nimetoka katika mji mtakatifu Yerusalemu". Zosima akauliza mara ya pili akasema: "Mama, Jangwani humu umekula nini?" Naye mwanamke akajibu: "Nilipovuka Yordani nilichukua mikate miwili na nusu. Lakini ilikauka upesi sana ikawa migumu kama mawe. Mikate hii ilinitosha kwa miaka kadha wa kadha." Zosima akazidi kuuliza akasema: "Mama, miaka yote hii hukupata taabu? Hukuona vishawishi katika moyo wako vya kutoka jangwani na kuwarudia watu?"

Mwanamke akamjibu Zosima akasema: "Nikikumbuka taabu na vishawishi vilivyoniipata jangwani hapa ninatetemeka kwa hofu hata sasa. Nikikusimulia taabu zangu na vishawishi vilivyonisumbua ninaogopa kuwa hata siku ya leo vitanishinda!" Lakini Zosima akamwomba akasema: "Mama, usinifiche neno! Kweli umenisimulia habari nyingi za maisha yako. Ninakuomba uendeleo kusimulia yote mpaka mwisho wala usiache neno lo lote!"

Basi mwanamke akaendelea kueleza akasema: "Usadiki, baba Zosima, muda wa miaka kumi na saba naliteswa kwa tamaa kali na mbaya **kabisa**. Nilipokula chakula changu cha humu jangwani nalitamani kula nyama au nalitamani kula samaki kama nilivyokula huko Misri. Nikaona kiu kali ya divai niliyopenda sana kwa kuwa zamani nilikunywa divai bila kiasi hata kulewa. Lakini jangwani hapa hata maji niliyakosa. Mara nyingi naliteswa kwa kiu iliyokuwa kama moto kinywani mwangu. Mara nyingi nalitaka kufa kwa kiu. Daima nilitamani kuimba nyimbo mbaya nilizoimba zamani. Maneno yao yamejaa na yamepanga kichwani na moyoni mwangu. Kila mara nikalia machozi nikapiga kifua changu nikakumbuka nadhiri yangu niliyomwekea Mama mtakatifu wa Mungu kabla ya kufika jangwani. Nikawaza kama ninasimama mbele ya sanamu ya Mama huyu mtakatifu niliyemchagua kuwa mlinzi wangu. Nikalia machozi nikasali. Nikamwomba ayafukuze mawazo haya mabaya yaliyosumbua roho yangu. Kila mara nilipokuwa nimelia machozi muda mrefu na baada ya kupiga vibaya kifua changu niliona nimeangaziwa kwa nuru ya ajabu na furaha ya kudumu ilinirudia. Lakini nitawezaje kukusimulia jinsi nilivyotaabika kwa mawazo machafu? Uniwie radhi, baba Zosima! Moto mkali uliwaka katika mwili wangu nao ukaamsha moyoni mwangu tamaa ya kurudia watu na uasherati. Basi hapo kila mara nikajitupa chini nikamwaga machozi mengi sana. Mara nyingi nalidhani kwamba Maria Mama wa Mungu amesimama kando yangu, maana ni mdhamini wangu. Akawa kama ananikaripia kwa sababu nalitaka kuvunja nadhiri yangu hata alinitisha kwa maneno yake. Kila mara nikawa nimelala chini mpaka nilipoona nuru ile ya ajabu iliyofukuza mawazo yaliyozungusha akili zangu. Moyo wangu ukamwelekea daima mwombezi wangu, Mama wa Mungu. Nikamsihi anisimamie kila wakati ili nidumu kukaa jangwani na kutubu. Naye Mama huyu mwema aliyemzaa Yesu aliye chemchemi ya usafi wa moyo hakuniacha kamwe. Amenilinda katika hatari zote zilizoniipata muda wote wa miaka kumi na saba!"

Zosima akamwuliza tena akasema: "Kumbe wewe huna mikate wala nguo?" Mwanamke akajibu akasema: "Mikate ile niliyochukua kutoka Yerusalemu ilinitosha kwa miaka kumi na saba kama nilivyokuambia. Baadaye nikala majani niliyoona jangwani. Mavazi niliyovuka nayo Yordani yakararukaruka. Wakati wa kiangazi nikataabika kwa joto la jua na wakati wa baridi nikakauka kwa baridi. Mara nyingi nilianguka kama nimekufa nikawa sikujimudu wala kupumua pumzi. Lakini nguvu ya Mungu imeniponya hata siku ya leo. Nikikumbuka kwamba Bwana ameniokoa na maovu yangu ninajiona nina nguvu. Nikiwaza wokovu wangu wa milele najiona nimeshiba. Ninajifunika kwa neno la Mungu mwenye kudumisha vitu

vyote. Mwanadamu chakula chake si mkate tu (Kum 8:3/Mt 4:4), na yule amevikwa vizuri aliyevua nguo ya dhambi!"

Zosima aliposikia mwanamke anataja maneno ya Maandiko Matakatiifu kutoka Musa, Ayubu na Zaburi, alimwuliza akasema: "Mama, wewe umesoma kitabu cha Zaburi na vitabu vingine vya Maandiko Matakatiifu?" Mwenzake akachekelea akasema: "Usadiki tu tangu siku ile nilipovuka Yordani sikumwona mtu usipokuwa wewe nimekuona leo. Pia sikumwona mnyama mkali. Tangu utoto wangu sikusoma wala sikumsikia mtu aliyenisomea. Lakini Neno la Mungu mwenye uhai na mwenye nguvu (Ebr 4:12), linawafundisha watu ndani yao. Basi, nimesimulia habari za kutosha za maisha yangu. Ninakuomba kwa ajili ya kuzaliwa kwa Mwana wa Mungu, uniombe mimi mkosefu mpootevu!"

Basi Zosima akamkaribia mwanamke akamwangukia miguuni pake akasema: "*Atukuzwe Mungu! Yeye peke yake atenda makuu na ya ajabu,*<sup>4</sup> yasiyofahamika na yasiyohesabika. Utukuzwe, wewe Bwana Mungu! Leo umenionyesha jinsi *unavyowatendea watu wanaokuogopa.*<sup>5</sup> Kweli, ee Bwana, huwaachi wale wanaokutafuta!"

Lakini mwanamke akamshika mzee Zosima, maana hakukubali ajiangushe mpaka chini akasema: "Ninakuapiza kwa Yesu Kristo, Bwana na Mkombozi wetu, usithubutu kueleza neno ulilosikia kwangu mpaka Bwana atakaponifungulia vifungo vya mwili wangu. Ukiniahidi kuzuia siri yangu hii, mimi ninakuahidi kukufikia tena mwaka ujao. Kwa msaada wa Bwana utaniona mara ya pili. Kwa upendo wa Bwana ufanye ninayokuagiza sasa: Mwaka ujao usitoke monasterini wala usivuke Yordani kama ilivyo desturi ya monasteri yenu!" Zosima akashangaa kwa kuwa mwanamke aliyajua mazoea ya monasteri yao. Akamsifu Mungu anayewapatia wapenzi wake zaidi kuliko yale waliyoomba (Efe 3:20). Mwanamke akaendelea akasema: "Basi, baba Zosima, mwakani ukae katika monasteri wala usitoke. Ijapokuwa utataka kwenda jangwani wakati wa Kwaresima, utashindwa kutoka nyumbani wakati ule. Lakini siku ya Jumatano inayotangulia Alhamisi kuu uchukue mwili mtakatifu wa Bwana na damu kidogo takatifu katika kalisi.<sup>6</sup> Uningojee kando ya Yordani, maana nitafika huko kupokea vipaji hivi vyenye uzima wa milele. Tangu nilipopokea sakramenti takatifu katika kanisa la Mtangulizi mtakatifu kabla sijavuka Yordani, sikupata tena neema hii. Utamwambia abate wako

---

<sup>4</sup> Zab 72:18

<sup>5</sup> Zab 31:19

<sup>6</sup> Katika Kanisa la Orhodosi waamini wanapokea Komunio kwa umbo la mkate uliochovywa katika kikombe cha divai. Padri anawapa mwili wa Kristo kwa kutumia kijiko.



Yohani kwamba mkosefu anakungoja kwenye Yordani. Lakini usimwambie sasa, ila wakati ule utakapoamriwa na Bwana!"

Kwisha kuagiza neno hili mwanamke aliomba baraka ya Zosima akatoka upesi. Zosima akajitupa chini akabusu mchanga aliosimama mwanamke. Akaanza safari ya kurudi katika monasteri akamsifu Mungu. Njiani hakuchoka kumtukuza Bwana Yesu Kristo na kumshukuru. Akapita njia ile ile aliyopita mara ya kwanza. Akafika monasterini wakati ule ule waliofika watawa wenzake wote. Mwaka mzima akaficha siri hiyo moyoni mwake. Lakini alisali kila siku Mungu amjalie kukutana mara ya pili na mwanamke yule. Siku zote alitamani kuonana naye lakini siku zilipita pole pole tu.

Dominika ya kwanza ya Kwaresima watawa wenzake walitoka tena nyumbani wakiimba zaburi wakaenda jangwani. Lakini baba Zosima hakutoka. Alikuwa mgonjwa wa homa akabaki monasterini. Akakumbuka maneno aliyosema mwanamke: "Hutaweza kutoka nyumbani ingawa utataka kutoka."

Wenzake wakarudi tena monasterini siku ya Jumatano inayotangulia Alhamisi kuu. Zosima akachukua Mwili mtakatifu wa Bwana na Damu kidogo takatifu katika kalisi na kikapu chenye tini na tende zilizokauka na choroko zilizowekwa. Kwa sababu hii alichelewa njiani. Akaketi kando ya Yordani akamngoja mwanamke mtakatifu. Huyu alipokuwa anakawia kufika Zosima hakuthubutu kulala usingizi bali alimtamazia jangwani. Akawa na wasiwasi akasema moyoni mwake: "Labda mwanamke alifika na amerudi tena kwa sababu hakuniona." Akalia machozi akamwomba Bwana akisali: "Ee Mungu wangu, unijalie kuonana naye. Sitatoka hapa mpaka nitakapomwona. Nitakaa hapa na nitatubu dhambi zangu."

Wakati alipokuwa anasali hali analia machozi lilimtokea wazo jingine: "Mama huyu mtakatifu akifika atafanyaje? Atavukaje Yordani kwa kuwa hamna mtumbwi? Atanifikiaje mimi mkosefu? Ole wangu, nikikosa kumwona mtakatifu huyu!"

Alipokuwa anafikiri hivi mwanamke mtakatifu alifika kutoka jangwani akasimama ng'ambo ya Yordani. Mzee Zosima akafurahi akamshangilia Mungu moyoni mwake (Efe 5:19). Akashikwa na uchungu kwa sababu hamna mtumbwi wa kuvukia. Mwezi mkuu ukaangaza sana nchi yote. Kumbe aliona kuwa mwanamke mtakatifu alipiga alama ya msalaba juu ya Yordani akashuka kwenye maji akapita juu ya maji kama anakanyaga nchi kavu. Zosima akamstaajabia akataka kupiga magoti. Lakini mwanamke aliyekuwa amefika katikati ya mto alimkataza. Akamwambia akipaza sauti yake akasema: "Baba Zosima, unafanya nini? Mbona wewe ni padre na umechukua Mwili mtakatifu wa Bwana!" Zosima akatii akaacha kupiga magoti. Mwanamke alipokwisha vuka na kumfikia alimwambia: "Baba, unibariki!" Zosima alikua ameshikwa

na bumbuazi kwa sababu ya mwujiza alioona, akabubujika akasema : "Mungu alisema kweli alipoahidi kwamba wale wanaojitakasa watafanana naye. Utukuzwe, ee Yesu, Mungu wetu!

Umenionyesha katika mjakazi wako huyu kuwa mimi ni mbali sana na ukamilifu!"



Mwanamke akamwomba Zosima asali sala ya Kanuni ya Imani na sala ya Bwana. Baada ya kupokea sakramenti takatifu kwa maumbo ya mkate na ya divai alinyanyua mikono yake akasali kwa ibada sana akasema: "*Ee Bwana, sasa umruhusu mtumishi wako kwa amani kama ulivyosema, kwa kuwa macho yangu yameuona wokovu wako!*" Lk 2:29-30.

Baadaye alimwambia Zosima akasema: "Uniwie radhi, baba, unikubalie neno moja: Urudi sasa katika monasteri yako kwa amani ya Mungu. Lakini mwaka ujao ufike tena pale pale tulipokutana safari ya kwanza. Ninakuomba kwa ajili ya pendo la Mungu, ufike tena huko. Utaniona pale pale akitaka Mungu." Zosima akajibu akasema: "Laiti ningekufuata sasa ili nizungumze nawe! Nami mzee ninaomba unikubalie neno moja: Uchukue chakula nilicholeta hapa!" Akamwonyesha kikapu alichoweka karibu. Kwa ncha za vidole vyake mwanamke akachukua choroko tatu akazitia kinywani. Akasema kwamba neema ya Roho Mtakatifu inamtosha kwa kumkinga dhambi. Halafu alimwambia mzee Zosima akasema: "Ninakuomba unisalie, ukumbuke upungufu wangu!" Zosima akabusu miguu yake akamwomba asalie kanisa na yeye mwenyewe akamruhusu kurudi jangwani.

Basi mwanamke mtakatifu akapiga tena alama ya msalaba akavuka akitembea juu ya maji kama mara ya kwanza. Mzee Zosima akarudi katika monasteri yake akawa amejaa furaha na hofu pia. Lakini alisikitika kwa sababu hakujuua jina la mwanamke yule mtakatifu. Akakusudia kuliuliza mwaka ujao akikutana naye.

Ulipopita mwaka Zosima alikwenda jangwani kama mwaka juzi ili aonane na mwanamke mtakatifu. Akapita jangwani pasipo njia. Lakini alishindwa kupaona mahali walipokutana mara ya kwanza. Akatazama huko na huko kama mwindaji anayetafuta mnyama. Alipokuwa haoni kitu alianza kulia machozi akatazama juu mbinguni akasali: "*Ee Bwana, ninakuomba unionyeshe malaika yule mwenye mwili!*"

Kwisha kusali alifika mahali palipofanana na pale alipokutana naye safari ya kwanza. Juu yake aliona mwanga wa ajabu kama mwanga wa jua. Alipokaribia pale aliona mwanga ule umetoka katika maiti ya mwanamke

mtakatifu aliyemtafuta. Alikuwa amefunga mikono yake juu ya kifua na kuelekea upande wa machweo ya jua. Zosima akamkaribia mbio akaosha miguu ya maiti kwa machozi yake. Hakuthubutu kugusa kiungo kingine. Baada ya kulia muda mrefu na kusali zaburi na maombezi alikusudia kumzika. Lakini alisitasita akifikiri: "Labda mtakatifu huyu hapendi kuzikwa nami." Alipowaza hivi aliona maneno yaliyoandikwa katika mchanga akasoma: "Baba Zosima, uizike maiti ya Maria mnyonge. Urudishie ardhi mali yake ukaweke vumbi lake ndani ya vumbi. Unisalie kwa Bwana. Nimekufa tarehe 9 Aprili, ni siku ya Mateso ya Bwana wetu, baada ya kupokea komunio takatifu."<sup>7</sup>

Mzee Zosima alitaka kumjua mtu aliyeandika maneno haya kwa kuwa mwanamke mtakatifu hakujua kuandika kama alivyosema mwenyewe. Akafurahi kwa sababu amepata kujua jina lake. Akatambua kwamba Maria huyu baada ya kupokea sakramenti takatifu kwenye Yordani saa ile ile alirudi mpaka hapa akafa pale pale. Zosima alitumia safari ya siku ishirini ya taabu sana kwa kufika hapa. Akamsifu Bwana, akalowanisha maiti kwa machozi yake. Halafu akasema: "Basi, nitimize yanipasayo. Lakini nifanyeje mbona sina chombo cha kuchimba kaburi? Sina jembe wala sepetu. Nimedhoofika kwa uzee na nimechoka kwa sababu ya safari wala sina nguvu." Alipokuwa anawaza hivi aliona kibao. Akakitwaa akaanza kuchimba kaburi. Lakini ardhi ilikuwa ngumu sana. Kwa hivi mzee Zosima alishindwa, maana alikonda kwa kufunga na amechoka kwa taabu za safari yake. Akajitahidi sana kuchimba akapumua kwa nguvu akawa anatoka jasho jingi sana bila kufaulu. Mara alipotazama maiti aliona simba mkubwa sana analamba miguu ya maiti. Zosima akatetemeka sana maana alimwogopa kabisa simba mkubwa huyu kwa kuwa marehemu alisema kwamba hajakutana na mnyama mkali. Akajiandikia alama ya msalaba pande zake zote akatumaini kuwa atanusurika kwa maombezi ya marehemu. Lakini simba akamkaribia Zosima kwa upole akalamba mikono na miguu yake kama anataka kumtuliza asiogope. Basi Zosima akamwambia simba akasema: "Wewe mnyama mkubwa sana umetumwa na Mungu kusaidia maziko ya mtumishi wake huyu. Basi ufanye kazi yako, chimba kaburi lake! Mimi mzee sina nguvu wala vyombo vya kufanyia kazi hii. Basi kwa amri ya Mungu chimba kaburi tupate kuzika maiti ya mtumishi mtakatifu wa Mungu!"

---

<sup>7</sup> Mwezi wa Pharmuthi kadiri ya kalenda ya Wamisri, Aprili kadiri ya kalenda ya Warumi, tarehe 9, yaani siku 5 kabla ya Idi ya Aprili, wakati wa Mateso ya Bwana Wetu Yesu Kristo. Kuhusu mwaka wengine wanafikiri kwamba alifariki mwaka 421

Kwa amri ya mzee Zosima simba alianza upesi kuchimba kaburi lililotosha kuzika maiti ya mtumishi mtakatifu wa Mungu. Zosima akaosha miguu yake mara ya pili kwa machozi yake. Akamwomba marehemu maombezi yake kwa ajili yake mwenyewe na kwa ajili ya watu wote. Baadaye akaweka maiti katika kaburi. Simba akamsaidia kufukia kaburi. Walipomaliza kazi hii wote wawili walitoka. Simba akaonkoka kama kondoo mpole akaendelea jangwani. Zosima akaanza kurudi katika monasteri yake. Njiani akamwambia Yesu Kristo nyimbo za kumsifu, akamtukuza Mungu akamshukuru. Alipofika monasterini aliwasimulia watawa wenzake habari zote za Maria huyu wa Misri tangu mwanzo mapka mwisho. Hakuficha neno lo lote alilosikia. Watawa waliosikia habari hizi walishangaa sana. Wakafanya ibada ya sikukuu kwa ajili ya mtakatifu huyu kwa hofu na upendo na imani.

Zosima akakaa katika monasteri ile mpaka alipotimia umri wa miaka mia moja. Akafariki dunia kwa amani ya Bwana na kwa neema ya Mkombozi Wetu Yesu Kristo, anayesifiwa na kuheshimiwa na kutukuzwa pamoja na Mungu Baba na Roho Mtakatifu sasa na sikuzote na milele. Amina.

Mt. Maria wa Misri, utuombee na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.<sup>8</sup>

---

<sup>8</sup> Kuhusu mwaka, wengine wanafikiri kwamba alifariki mwaka 522 au 530, yaani karne moja baadaye. Sikukuu ya Maria mtakatifu wa Misri hufanywa tarehe 2 Aprili katika Kanisa Katoliki. Amekufa mwaka 421 baada ya kuzaliwa Bwana Wetu Yesu Kristo.

## **Taisi Mtakatifu**

### **Aliyekuwa Kahaba**

#### **Sura ya I**

Taisi alizaliwa katika mji mdogo fulani wa nchi ya Misri. Wazazi wake walikuwa Wakristo wema. Kwa mapenzi ya Mungu wakafa Taisi angali bado mtoto mdogo.

Taisi alipokua akaonekana kuwa msichana mwenye uzuri wa ajabu wa umbo na sura yake. Lakini Taisi alikitumia kipaji hiki cha Mungu vibaya. Alipenda kustaajabiwa na watu kwa ajili ya haiba yake na kusifiwa kwa sababu ya uzuri wake. Akafanya umaridadi mwingi ili azidi kuwapendeza watu. Kwa hivi hakukawia kupoteza uzuri wa roho yake aliopewa katika ubatizo. Alipokwisha haribika hakupenda kukaa tena kwa jamaa yake, akatoroka. Akaenda pwani akakaa katika mji wa Aleksandria ulio mji mkubwa sana kando ya bahari ya katikati.

Sifa yake mbaya ikaeneza upesi sana katika mji ule walipokutana watu wabaya wengi sana. Hao wakamfikia kwa tamaa ya kutenda dhambi na mwanamke mzuri huyu. Taisi akapewa mali nyingi sana za dhambi. Akavaa mavazi bora ya hariri, akajipamba kwa marembo ya lulu na ya dhahabu. Kwa njia hii alizidi kuwatamaisha vijana wengi sana. Mara nyingi ikatukia kuwa watu waliomfikia Taisi nyumbani kwake walipigana hata waliuana, kwa sababu ya kuoneana wivu.

Basi habari hizi za kahaba huyu Taisi zikasikilika hata jangwani. Kule alikuwako mtu, jina lake Pafnusi, naye alikuwa mkaa pweke tangu miaka mingi. Pafnusi huyu akasikia habari za ubaya wa Taisi. Akasikitika sana kwa sababu kiumbe huyu anamkasirisha Baba yake wa mbinguni kwa kuvitumia vibaya vipaji vile vile alivyopewa naye. Akaogopa kuwa mwisho Taisi, asipoacha kutenda dhambi, atapotea milele. Akamwomba kwa sala zake. Akajisumbua vibaya, kwa njaa na kiuu na kwa mambo magumu mengine, ili amwombe huruma kwa Mungu Baba. Lakini Pafnusi hakupata raha moyoni mwake akiwaza kwamba Taisi atatengwa milele na Muumba wake. Basi akakusudia kumwoko katika dhambi zake. Siku moja Pafnusi akavua mavazi yake ya kitawa akavaa mavazi ya kidunia. Akachukua kipande cha dhahabu na akatoka jangwani kumwendea Taisi nyumbani kwake huko Aleksandria. Akamkuta kwenye baraza ya nyumba yake. Pafnusi akajisingizia kama anamtamani sana, akampa kipande kile cha dhahabu kuwa mshahara wa

dhambi. Taisi akakipokea akamwambia Pafnusi akasema: “Basi, twende nyumbani!”

Pafnusi akamfuata Taisi mpaka nyumbani. Wakaingia chumbani kwenye mapambo mazuri na kitanda. Pafnusi akawa anatazama huko na huko akionyesha kama anahangaikia mlango na madirisha. Akamwuliza Taisi : “Je, kuna chumba kingine pembeni zaidi na pasipo madirisha ? Tafadhali kama kiko twende huko huko!” Taisi akamjibu akasema: “Kiko, lakini usiogope, hata katika chumba hiki watu hawawezi kutuona wala hakuna mtu atakayeingia humu. Lakini ukimwogopa Mungu, ujue kuwa hatuwezi kujificha machoni pake!”

Basi Pafnusi akamwuliza Taisi akasema: “Je, wewe unajua kuwa Mungu yuko?” Taisi akajibu akasema: “Ndiyo najua kwamba Mungu yuko. Pia najua kuwa watu wema watapata maisha ya milele, bali wakosefu watapata mateso ya milele.”

Pafnusi akamwitikia akasema: “Ndivyo itakavyokuwa! Je, kwa sababu gani wewe umeziharibu roho za vijana wengi hivi? Wewe utahukumiwa na utalaaniwa milele kwa sababu ya dhambi zako, pia kwa sababu ya dhambi za wale uliowaharibu kwa ubaya wako!”

Taisi aliposikia maneno haya alimwangukia Pafnusi akashika miguu yake hali anatokwa na machozi mengi. Akamsihi mkaa pweke aliyetoka jangwani kwa ajili yake akasema: “Baba, unipe adhabu ya kutubisha. Uniombe mimi mkosefu mbaya, ili nipate matumaini ya kusamehewa dhambi zangu; Ninakuomba unipe muda wa saa tatu. Baadaye nitakuwa tayari kufika mahali utakaponiagiza na kufanya utakayoni amuru!”

## Sura ya II

Pafnusi akamwagiza mahali watakapokutana, akatoka. Taisi, lakini, akachukua mali zake zote, yaani mavazi na urembo na mapambo yaliyofanywa kwa fedha na dhahabu. Akavipeleka vitu hivi vyote sokoni bila kuangalia mshangao na dhahabu za watu aliowakuta njiani. Akavitupa vyote katika moto uliowaka sokoni. Akatangaza kwa nguvu yote ya sauti yake akasema: “Ninyi nyote mliotenda dhambi pamoja nami, njoni na mtazameni: ninateketeza vyote mlivyonipa!”

Vilipokwisha unguwa vyote Taisi alikwenda mahali alipoagizwa na Pafnusi. Huyu akamtangulia wakaenda katika konventi. Akamwingiza Taisi katika kijumba kidogo akafunga mlango akavuta kifungio na kukitia muhuri. Akaacha dirisha dogo katika mlango ili watawa wapate kumpa chakula.

Akamwagiza Mkuu wa watawa kwamba Taisi apewe kipande kidogo cha mkate na birika la maji kila siku.

Pafnusi alipotaka kurudi Taisi akamwuliza akasema: “Je, Baba, nisali nini kijumbani humu?” Pafnusi akasema: “Wewe hustahili kumtaja Mungu, na midomo yako isitamke hata jina lake takatifu, wala usiinue mikono yako mbinguni! Midomo yako na mikono yako imechafuka. Ujiiamishe upande wa maawio ya jua na kusema kila mara: ‘Ewe uliyeniumba, unihurumie!’”


### Sura ya III

Ikapita miaka mitatu. Pafnusi akamkumbuka Taisi akamwonea huruma. Kwa hivi akamwendea Antoni mtakatifu amwulize kama Mungu amesamehe dhambi Taisi. Antoni akawakusanya pamoja wanafunzi wake wote. Akawaagiza wote wakeshe usiku kucha na wasali, ili Mungu amfumbulie mmoja wao neno alilouliza Pafnusi.

Basi kila mwanafunzi akaenda katika kijumba chake na kukesha na kusali. Katika kundi la wanafunzi hawa alikuwa mtawa aliyelitwa Paulo mjinga. Huyu alikuwa mtawa mwema sana na mwanafunzi hodari kweli wa Antoni mtakatifu. Paulo huyu alipokuwa akisali usiku ule aliona maono.

Aliona kiti kilichopambwa kwa ajabu sana. Kiti hiki kimelindwa na mabikira watatu wenye kung’aa sana. Paulo mjinga akistaajabia kiti pamoja na mabikira wale, akawaza moyoni mwake : “Hakika kiti hiki kitakuwa kiti cha baba yangu Antoni katika utukufu wa mbinguni!” Kumbe pale pale sauti kutoka mbinguni ikasema: “La, kiti hiki hakitakaliwa na baba yako Antoni. Kiti hiki ni cha Taisi mwenye kutubu dhambi zake.”

Asubuhi, walipokutana watawa wote, Paulo mjinga akawasimulia njozi yake. Basi Pafnusi akapokea neno la Mungu lililomhusu Taisi, akiwa ana uhakika kwamba Mungu amesamehe. Akaenda Aleksandria katika konventi alimofungwa Taisi. Akafungua mlango wa kijumba chake. Taisi akaomba akasema: “Tafadhali msifungue mlango! Mniache nikae humu!” Pafnusi lakini akafungua mlango na kwa furaha kubwa alimwambia Taisi akasema: “Utoke sasa, maana Mungu amekusamehe dhambi zako!”



za

Taisi akamwangukia Pafnusi miguuni pake akasema: “Ninashuhudia mbele ya Mungu: Tangu nimeingia humu sikuacha kukumbuka dhambi zangu. Zikawa kama mlima machoni pangu. Nikaona uchungu katika moyo wangu wala sikuacha kulia machozi siku zote.” Pafnusi akamwambia kwa upole : “Mungu amekusamehe dhambi zako zote, kwa sababu ulizikumbuka kwa uchungu wa moyo wako!”

Wakamtoa Taisi. Naye akampokea Mkombozi wake katika sakramenti takatifu.

Pafnusi akatoka akarudi jangwani. Baada ya majuma mawili Taisi akafa katika amani ya Bwana.

Mt. Taisi, utuombe na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

Sikukuu yake hufanywa tarehe 8 Oktoba.



## **Mtakatifu Martha wa Kairo Mtubu**

Martha alizaliwa katika mji wa Mesr, Kairo, Misri. Wazazi wake walikuwa tajiri. Tangu ujana wake akaishi maisha ya umalaya na akajulikana sana. Lakini kwa neema ya Mungu, akasukumwa siku moja kwenda kanisani. Ilikuwa sikukuu ya Krismasi, yaani Kuzaliwa Bwana wetu Yesu Kristo. Alipokaribia penye mlango wa kanisa, bawabu akamzuia kuingia akisema: “Haifai kwa mtu kama wewe kuingia katika kanisa takatifu. Unajua wewe ni nani.” Wakabishanabishana. Askofu aliposikia kelele akaja kuuliza kulikoni. Alipomwona msichana huyu akamwambia: “Hujui kwamba Kanisa ni mahali patakatifu na wale tu waliotakaswa wanaweza kuingia?” Martha akalia na kumwambia: “Baba unipokee, sasa hivi ninatubu dhambi zangu, na nimeamua kutorudi katika maisha ya zamani”.

Askofu akamjibu: “Kama ni kweli unayosema, nenda na uniletee mavazi yako ya hariri na mapambo yako ya dhahabu.” Akakimbia haraka na kuviletea Askofu. Askofu akaamua vichomwe moto. Basi akanyolewa nywele zake, akavishwa na vazi ya kitawa na akamtumwa kukaa kati ya monasteri mojawapo.

Akapiga vita ya ki-roho kwa nguvu zake zote na mara nyingi alikuwa akisema: “Bwana, kama sikuweza kuvumilia aibu ya mtumishi wa Nyumba yako, tafadhali usiniaibishe mbele ya Malaika na Watakatifu wake.” Akaendelea kupiga vita ya ki-roho kwa miaka ishirini na tano. Na kwa wakati wote hakutoa nje ya monasteri hata mara moja. Akafariki kwa amani.<sup>9</sup>

Mt. Martha, utuombea na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

---

<sup>9</sup> *Ethiopian Synaxarium: Senne 03*. Siku hiyo ndiyo tarehe 10 mwezi wa Juni katika kalenda yetu. Wakoptiki wa Misri wanamkumbuka tarehe 28 mwezi wa Mei.

## Mtakatifu Theodora wa Aleksandria Mtubu



Zamani za Zeno, Kaizari wa Roma, Mt. Theodora na mume wake waliishi Aleksandria, mji mkuu wa Misri wakati ule. Upendo na amani vilitawala familia yao, na hiyo ndiyo ilisababisha chuki kubwa ya Adui wa wokovu. Kwa kuongozwa na Shetani, mtu tajiri, Shuja, alihangaishwa na uzuri wa Theodora na akaanza, kwa kutumia mbinu zake zote, zawadi na barua, kumtongoza ili azini naye. Kwa muda mrefu hakufaulu. Mwishoni akamhonga mwanamke wa sifa mbaya, akamwahidia zawadi kubwa akifaulu kubadilisha nia yake. Basi mwanamke huyu akamwendea Theodora na kusihi kumhurumia mtu huyu tajiri na kukubali kutimiza haja yake. Theodora akamjibu kwamba Mungu anaona kila kitu na hayupo tayari kutenda dhambi kubwa kama hiyo. Basi mwanamke akamdanganya Theodora kwa kumwambia kwamba dhambi iliyotendeka sirini, ambayo Jua haliioni, ni dhambi Mungu haijui. Theodora akamwuliza, “Unaniambia

kweli ?” “Ndiyo nakuambia ukweli”, mwanamke akamjibu. Basi Theodora alipodanganywa akakubali. Akamwambia mwanamke: “Mwanaume huyu afike usiku huu nitakubali kutimiza hamu yake.” Mwanamume akafurahi, akafika saa alipoambiwa na kutimiza haja yake. Theodora akamsaliti mume wake. Lakini mara akajitambua na alipoona ubaya wa kosa lake, akakasirika, akajipigapiga na kuchana nywele zake. “Ole wangu, nimepotea, nimeharibu uzuri wa jina langu.” Mume wake akaingia, akamwona mke wake akilialia. Akataka kujua sababu ya huzuni yake, lakini hakutaka kumwambia. Usiku kucha dhamira yake haikumpatia amani.

Asubuhi mapema akaenda kwa Mama Mkuu wa konventi, akamwuliza ikiwa Mungu anajua dhambi yoyote iliyotendeka usiku. Mama Mkuu akamjibu kwamba hakuna kitu kilichofichika kwa Mungu. Theodora akalia sana, akamwambia yote. Mama Mkuu alipoona kwamba Theodora anaonyesha toba kweli, akamweleza msamaha wa Mungu na kumkumbusha dhambi ya uzinzi ya mwanamke aliyeosha miguu ya Yesu kwa machozi yake na kupokea kutoka kwake msamaha wa dhambi zake.<sup>10</sup> Kwa kutamani huruma ya Mungu,

---

<sup>10</sup> Rejea Lk 7:36-50

Theodora akasema: “Namwamini Mungu wangu, na tangu saa hii, sitatenda dhambi ya namna hiyo, na nitajitahidi kumlipia kosa.”

Muda si muda, siku moja mume wake alipotoka, akakata nywele zake, na akivaa mavazi ya mume wake akaondoka kisirisiri, akaenda kwa monasteri<sup>11</sup>, umbali wa kilomita 30 na nyumba yake, kwa sababu aliogopa kwamba mume wake atamtafuta katika konventi.

Abate, ili kumjaribu kandidati mpya, hakutaka hata kumbariki kwa kuingia uani. Basi usiku ule Theodora akalala kwenye mlango. Asubuhi mapema, akamwangukia magotini mwa Abate na kumwambia kwamba jina lake lilikuwa Theodori kutoka Aleksandria. Akamsihi aingie monasteri ili atubu na kufanya kazi. Alipoona nia yake nzuri, Abate akakubali. Theodora akafurahi, akajiita Theodori na mara akaanza kufuata sheria zote za monasteri kwa bidii sana. Hata watawa walioishi humo miaka mingi, wakashangaa kumwona mtawa Theodori akikeshwa usiku mzima magotini, na kuona unyenyekevu wake, saburi yake na kujikana kwake. Mtawa Theodori akafanya kazi kwa miaka minane. Mwili wake, ulionajisiwa siku moja kwa dhambi ya uzinzi, sasa ulianza kuwa chombo cha neema ya Mungu, na hekalu la Roho Mtakatifu.

Siku moja, Mtawa Theodori alitumwa kwenda mji wa Aleksandria kununua mafuta. Akasafiri. Mume wake alikuwa amelia sana. Aliogopa kwamba ametoroka na mwanamume mwingine. Malaika akamtokea na kamwambia, “Amka mapema, nenda katika njia ya Watakatifu Petro na Paulo, na yule utakayemwona, ndiye mke wako”. Basi mtawa Theodori akaja na ngamia wake. Alipomwona mume wake kwa mbali, akasema moyoni mwake, “Mume wangu mwema, ni kazi gani za toba inanipasa kuzitenda ili nipate msamaha wa dhambi niliyokutendea?” Alipokaribia akamsalimu, “Bwana Mungu akujalie furaha, bwana wangu”. Hakumtambua mke wake. Baada ya kurudi nyumbani sauti ikamwambia, “Aliyekusalimu, alikuwa mke wako!”

Mtawa Theodori alizidi kukua katika utakatifu. Akafanya miujiza mingi. Kwa sala zake akamwoko mwanamume mmoja aliyeraruliwa na mnyama wa pori. Akamlaani mnyama, na mara moja mnyama yule akaanguka na kufa. Shetani hakuweza kuvumilia utakatifu wake. Akamtokea na kumwambia: “Wewe Malaya kuliko wote, mzinzi, umemwacha mume wako na kufika hapa kunidharau. Kwa nguvu na uwezo wangu nitakupigia vita na kukufanya kwamba utamkana Yesu Kristo msulubiwa.” Mtawa Theodori akafanya ishara ya msalaba, na mara Shetani akatoweka.

---

<sup>11</sup> Monasteri ni nyumba ya watawa wanaume kwa wanawake lakini konventi ni nyumba ya watawa wanawake tu.

Siku moja alipotumwa kutafuta chakula mjini, baada ya kumbariki kwa ajili ya safari yake, Abate akamwambia, “Kama unachelewa, basi ulale katika monasteri huko Enata, ambayo iko njiani.” Kumbi binti wa Abate wa monasteri ile alikuwa pia katika guest house ya monasteri. Alifika kumtembelea baba yake. Alipovutwa na uzuri wa mtawa huyu, akajaribu kumtongoza mtawa Theodori kwa dhambi ya uasherati, asijue kwamba ni mwanamke anayekaa mbele yake. Alipokataliwa basi akaenda kuzini na mgeni mmoja aliyekuwa pia katika guest house hiyo. Akapata mimba. Wakati ule mtawa Theodori akarudi nyumbani na kuleta vyakula.

Baada ya muda, baba yake msichana huyu akatambua kwamba ana mimba, akaanza kumhoji ili kujua baba ya mtoto ni nani. Msichana huyu akamwambia baba yake kwamba nidye mtawa Theodori. Mara moja, Abate wa monasteri ya Enata akampasha habari Abate wa monasteri ambayo Mtawa Theodori alikuwa anajitahidi kwa kufanya toba. Abate akamwita na kumweleza Mtawa Theodori. Mtakatifu akamjibu: “Mungu awe shahidi wangu, sikufanya tendo hilo.” Abate akijua usafi wa moyo na utakatifu wa Mtawa Theodori hakuamini mashtaka haya. Muda ukapita, msichana akajifungua, mtoto wa kiume. Punde si punde Watawa wa Enata wakamleta mtoto kwenye monasteri Mtawa Theodori alipokaa. Wakaanza kumkaripia mtawa Theodori kwa sababu ya uzinifu wake. Wakatumia maneno mengi kwa nguvu nyingi, hata Abate wa Theodori akaanza kuamini maneno ya watawa wa Enata na kumkasirikia. Wakamkabidhia mtawa Theodori mtoto na wakamtupa nje ya monasteri, kwa aibu.

Mtakatifu akakubali majaribio haya mapya, akiyaona kuwa sehemu ya kutakaswa na dhambi ya zamani. Akaishi katika kibanda, siyo mbali na monasteri. Wachungaji, wakimhurumia, wakampa maziwa kwa ajili ya mtoto, na yeye mtawa Theodori akala majani ya pori.

Shetani akimwonea wivu kwa uvumilivu wake akamtokea mtawa Theodori kwa umbo la mume wake. Akamwambia, “Njoo, rudi sasa nyumbani. Nimekusamehe dhambi yako.” Naye, akifikiri kwamba kweli ni mume wake, akamjibu, “Sitakaa tena pamoja nawe, kwa sababu mwana wa Yohane, Shujaa (*Knight*) amezini nami. Nitafanya toba kwa dhambi hiyo niliyokutendea mpaka mwisho wa maisha yangu.” Akamwomba Mungu na Shetani akatoweka. Hakumtambua kwamba mwanamume huyu ndiye Shetani.

Shetani akizidi kukasirika, akatumia nguvu zake kumtisha. Pepo wengi wakamjia kwa umbo wa wanyama wakali na mtu fulani akawaambia, “Mle Malaya huyu”, lakini Mtawa Theodori akaomba na mara wakatoweka. Wakati mwingine tena washujaa wengi wakamfikia, kati yao alikuwepo Mfalme. Washujaa wote walikuwa wanamwabudu. Washujaa wakamwambia Mtawa

Theodori, “Inuka na umwabudu Mfalme wetu.” Akawajibu, “Namwabudu Bwana Mungu wangu.” Mfalme alipoambiwa hayo, akawaamuru washujaa wake wamlete kwake, na kumtesa na mateso mengi hata kuachwa kama mfu. Mtawa Theodori akaomba na wote wakatoweka. Wakati mwingine akaona dhahabu nyingi. Akaibariki na kuikabidhi kwa Mungu. Yote yakatoweka. Tena wakati mwingine akaona kikapu kimejaa na chakula bora, nyama, samaki, mboga, matunda na mambo mengine. Akasikia sauti ikisema, “Mfalme aliyekupiga anakuumuru kukichukua na kukila, kwa sababu alifanya hivyo bila kukusudia”. Akaibariki na yote yakatoweka.

Baada ya miaka saba, kwa ruhusa ya Abate, akarudi kuishi katika nyumba ya watawa, pamoja na mtoto. Siku moja, Abate akaangaziwa na Mungu kwamba dhambi ya mtawa Theodori imesamehewa. “Neema ya Mungu i juu ya mtawa Theodori, na karibuni hivi, watawa wote watashuhudia kazi zinazotendwa kwa njia ya sala ya Mtakatifu huyu.”

Ikatokea kwamba wakati wa ukame visima vyote vilikauka. Abate akawaambia watawa kwamba mtawa Theodori tu ataweza kubadilisha balaa hiyo. Akimwita mtakatifu, Abate akamwambia kuleta maji. Mtawa Theodori akaenda kuchota maji katika kisima kimoja na akayampelekea Abate. Tangu siku ile maji hayakukauka kamwe katika kisima kile. Kwa unyenyekevu mtawa Theodori alisema kwamba mwujiza huu uliletwa kwa njia ya sala na imani ya Abate.

Kabla ya kifo chake, mtawa Theodori akajifungia ndani ya chumba chake, pamoja na mtoto. Abate alipopata habari akamtuma mtawa kusikiliza anachosema. Mtawa akaingia na akamsikia mtawa Theodori akimfundisha mtoto kumpenda Mungu kuliko mambo yote. Akamwambia pia kumtii Abate na watawa, ili kukaa katika amani, kuwa mpole na bila hila, kuepuka upujufu na upuuzi, kutotamani, na kutokosa sala za pamoja. Baada ya hayo, akasali na kwa mara ya mwisho akamwomba Mungu amsamehe dhambi zake. Mtoto akasali pia pamoja naye. Mara maneno ya sala yake yakafifiwa midomoni mwake, na kwa amani akaaga dunia kuelekea makao bora. Ilikuwa mwaka 460.

Usiku ule Bwana Mungu akamfunulia Abate katika maono, mambo yote mtawa Theodori aliyoyafanya, na pia siri yake. Abate, ili kuondoa aibu juu ya mtawa Theodori, mbele ya Abate wa monasteri ya Enata na watawa wake wote, akawaambia maono yake. Alipomaliza maneno yake, akavua nguo iliyofunika maiti ya mtawa Theodori, na wote wakathibitisha kwa macho kwamba yeye alikuwa mwanamke.

Abate wa monasteri ya Enata na watawa wote wakahangaika wakikumbuka makosa yao. Wakamwangukia maiti ya mtakatifu, kwa machozi na

kumwomba msamaha. Habari za kifo cha Theodora zikamfikia mume wake wa zamani. Akafika kuhudhuria mazishi yake na pale pale akajiunga na watawa, na kuishi katika chumba kidogo kile kile mke wake alimoishi. Mtoto huyu pia akawa mtawa na baada ya miaka akawa Abate wa manasteri ile.<sup>12</sup> Mt. Theodora, utuombe na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

\*\*\*\*\*

---

<sup>12</sup> Katika Kanisa Katoliki sikukuu yake inaadhimishwa tarehe 11 Septemba.

## Mt. Pa'esa, Mwanamke aliyetubu

Mwanamke huyu alizaliwa huko Menouf, Misri kwa wazazi wacha Mungu. Alipofiwa na wazazi wake alirithi mali yao. Akageuza nyumba yake kuwa kikimbilio cha maskini na wapita njia. Alipokea kila mmoja mwenye mahitaji na kumhudumia mpaka fedha zake zikaisha. Ndipo watu wabaya wakamshauri na kufaulu kubadilisha mawazo yake. Akageuza nyumba yake kuwa danguro. Habari hizo zilipowafikia wazee wa Shete, walisikitika sana. Wakamwita Mt. Yohane mfupi, na kumwomba aende kumtembelea, kama tendo la huruma, ili kumsaidia kuokoa roho yake, kwa ajili ya matendo mema aliyowatendea watu. Mtakatifu akakubali na kuomba msaada wao wa sala. Alipofika nyumbani mwake, akamwita mjakazi mmoja kutangaza ujio wake. Kwa habari hiyo Pa'esa akajipamba na kumwita aingie. Akiingia Yohane akasema moyoni mwake: *“Naam, nijapopita kati ya bonde la uvuli wa mauti, sitaogopa mabaya, kwa maana wewe upo pamoja nami”* Zab 23:4. Akaketi, akamkazia macho Pa'esa na kumwambia: *“Kwa nini ulimdhaliisha Bwana Yesu Kristo na kutenda uovu huo?”* Pa'esa akatetemeka na moyo wake ukayeyuka kwa maneno yake. Yohane akainama kichwa chake na kuanza kulia machozi. Akamwuliza: *“Kwa nini unalia?”* Akamjibu: *“Kwa sababu naona pepo wanavyocheza usoni mwako, kwa hiyo ninakulilia.”* Pa'esa akamwuliza: *“Je, kuna toba kwa ajili yangu?”* Akamjibu: *“Ndiyo, lakini siyo mahali hapa”*. Basi Pa'esa akamwambia: *“Unichukue mahali popote upendapo”*.

Basi akampeleka kwa moja wa nyumba ya watawa wa kike jangwani mwa Shete. Njiani usiku ukawafunika. Yohane akamwambia Pa'esa kulala mahali fulani, wakati yeye atajilaza mbali kidogo. Aliposimama ili kusali sala za usiku, akaona nguzo ya mwanga ikishuka kutoka mbinguni na malaika wakibeba roho ya Pa'esa. Akamkaribia Pa'esa na kuona kwamba amekwisha fariki. Akapiga magoti na kuomba kwa nguvu, hata machozi yakamtokea, akimwuliza Mungu kumwambia ukweli kuhusu wokovu wake. Akasikia sauti ikisema: *“kutubu kwake kulipokelewa wakati alipotubu.”* Baada ya kumzika maiti yake, akarudi kwa wazee na kuwaambia yote yaliyotokea. Wakamsifu Mungu anayewapokea watubu na kuwasamehe dhambi zao.<sup>13</sup>

Mt. Paesa, utuombe na Mungu atukuzwe daima na milele. Amina.

---

<sup>13</sup> Kutoka Coptic Synaxarium: 2 Misra.

## WASIA

Ningependa kumaliza habari hizo kwa kunakulu hadithi moja iliyandika na ndugu Palladius, katika Kitabu chake: “*The Lausiatic History*”.

Bikira mmoja pamoja na wenzake wawili, walikuwa wakitenda majikanio (*ascetism*) kwa miaka tisa au kumi. Siku moja akashawishiwa na Mhudumu. Akaanguka na kupata mimba na kumzaa mtoto. Akaanza kumchukia sana baba ya mtoto, kiasi kwamba akashtakiwa na dhamira yake, akatubu lakini akakata tamaa na kutamani kufa. Akaanza kujinyima chakula ili afe. Katika kusali kwake akamwomba Mungu hivi: “Mungu Mweneyzi, wewe unayajua maovu ya kila kiumbe, hutaki kifo wala ungamizi wa wale wanaoanguka, ukitaka niokolewe unionyeshee maajabu yako, umchukue mtoto huyu tunda la dhambi yangu. Kama sivyo najinyonga au najitupia kujiuu.”

Mungu akasikia sala yake. Muda si muda mtoto akafariki. Tangu siku hiyo hakumkuta tena baba ya mtoto aliyemfunga katika vifungo vyake. Akajitolea kabisa kuwatumia wagonjwa na vilema. Akafunga vibaya sana kwa miaka thelathini. Akamsumbua Mungu kiasi kwamba Padri mmoja akafunuliwa na Mungu: “Fulani ananipendeza zaidi katika toba zake kuliko katika ubikira wake.”<sup>14</sup>

Naandika hayo ili tusiwahukumu wenyedhambi wala kuwadharau wale wanaotubu kweli kweli.

\*\*\*\*\*

---

<sup>14</sup> Palladius: *The Lausiatic History*, sura LXIX